JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA**


Simu Nambari: 2152532/3
Baruapepe: cg@dcea.go.tz
Tovuti: www.dcea.go.tz
Nukushi: 2152820

8Barabara ya kivukoni
S.L.P. 80327
Dar es Salaam
Tanzania


## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

## TAARIFA YA HALI YA DAWA ZA KULEVYA NCHINI KWA MWAKA 2019.

**Dodoma, 10 Juni 2020**:

Matumizi na biashara ya dawa za kulevya ni tatizo linaloiathiri dunia licha ya jitihada za udhibiti zinazofanyika. Kwa mujibu wa Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya Duniani ya mwaka 2019 (Word Drug Report 2019), takribani watu milioni 271 ambao ni asilimia 5.5 ya watu wenye umri wa miaka 15 hadi 64 walitumia dawa za kulevya mwaka 2017. Mfumuko wa dawa tiba zenyye asili ya kulevya pamoja na uchepushwaji wa kemikali bashirifu kutoka katika mfumo halali wa kutengeneza dawa za kulevya, vimechangia kwa kiwango kikubwa uwepo wa dawa za kulevya na ongezeko la watumiaji wa dawa hizo duniani.

Katika kipindi cha mwaka 2019, Matumizi na biashara ya dawa za kulevya liliendelea kuwa ni tatizo hapa nchini pia. Pamoja na kuwa bangi ilikuwa dawa za kulevya iliyotumika zaidi hapa nchini katika kipindi hicho, pia kulijitokeza ongezeko la matumizi ya dawa tiba zenye asili ya kulevya kama vile Tramadol, Ketamine, Valium na zinginezo. Ongezeko hili lilichangiwa na udhibiti mkubwa wa dawa za kulevya zilizozoeleka kama vile heroin na cocain unaofanywa na serikali. Waraibu wa dawa za kulevya wanapokosa dawa walizozizoea hukimbilia kutumia dawa tiba zenye asili ya kulevya ili kupunguza makali ya arosto wanayoipata.

Serikali kwa kupitia Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya imepata mafanikio makubwa katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya hapa nchini kwa

mwaka 2019. Kwa kushirikiana na wadau wa nje na ndani ya nchi, imefanya operesheni mbalimbali ndani ya nchi ikiwemo mipakani na katika ukanda wa Pwani na Bahari ya Hindi na kufanikiwa kwa kiasi kikubwa kupunguza uingizwaji wa dawa za kulevya nchini. Kwa mwaka 2019, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ilikamata jumla ya kilogramu 55.35 za heroin, kilo 10.34 za cocaine, tani 21.16 za bangi na tani 9.07 za mirungi ikiwahusisha watuhumiwa wapatao 10,384 ambao kesi zao ziko katika hatua mbalimbali mahakamani.

Dawa za kulevya zinazokamatwa huteketezwa kwa mujibu wa sheria kwa kushirikisha Mamlaka mbalimbali za Serikali baada ya hukumu kutolewa. Mwaka 2019 tuliteketeza kilo 122.55 za heroin na kilo 71.507 za cocaine katika viwanda vya saruji Dar es Salaam na Mbeya.

Katika kukabiliana na madhara yatokanayo na matumizi ya dawa za kulevya, Serikali imeendelea kuimarisha huduma za tiba kwa waraibu wa dawa za kulevya ambao hadi mwezi Desemba mwaka 2019 serikali imeanzisha vituo sita vya kutolea matibabu kwa waraibu wa dawa za kulevya kwa kutumia Methadone. Vituo hivyo vilivyopo katika mikoa ya Dar es Salaam, Mbeya, Mwanza, na Dodoma vilikuwa vimesajiri waraibu wapatao 7,600. Aidha, Serikali iliendelea kuratibu huduma za upataji nafuu kwa waathirika wa dawa za kulevya katika nyumba za upataji nafuu (Sober houses) ambapo waraibu wapatao 3,600 waliweza kuhudumiwa, hivyo kufanya idadi ya waraibu waliohudumiwa mwaka 2019 kufikia zaidi ya 11,100.

Dawa za kulevya ni tatizo mtambuka ambalo linaathiri jamii ya watanzania katika nyanja zote muhimu za kiafya, kijamii, kiuchumi, kimazingira na hata kwa upande wa diplomasia. Matumizi na biashara ya dawa za kulevya yameathiri maeneo mbalimbali ya nchi yetu kuanzia mijini hadi vijijini.

Watumiaji wa dawa za kulevya huhatarisha afya zao ikiwemo vifo vya ghafla, kupata maradhi yanayoambukizwa kwa njia ya damu ikiwemo VVU na homa ya ini aina C.

Inakadiriwa kuwa katika kila wajidunga wanane (8) mmoja anaishi na maambukizi ya VVU. Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia MAambukizi ya VVU na UKIMWI

(UNAIDS) limekadiria kuwa mjidunga anauwezako mara 22 zaidi ya kuambukizwa VVU ikilinganishwa na watu wengine kwenye jamii.

Kumekuwa na matumizi ya dawa za kulevya miongoni mwa wanawake. Wanawake wanaotumia vilevi wanavitumia kwa haraka zaidi kuliko wanaume na hupata uraibu wa madhara mengine yanayotokana na matumizi ya dawa za kulevya kwa haraka zaidi kuliko wanaume. Hata hivyo, wanawake waliothirika na dawa hizo hupata woga kujitokeza kwenye huduma za matibabu ya uraibu.

Matumizi ya dawa za kulevya kwa wajawazito husababisha athari kwa watoto wao na wanapojifungua na huathiri familia zao kwa kiwango kikubwa zaidi kwa kushindwa kuwapa malezi bora watoto wao. Watoto na wanawake hawa wako kwenye hatari kubwa ya kujiingiza kwenye matumizi ya dawa za kulevya. Hali hii inatengeneza vizazi vya waraibu wa dawa za kulevya .Hali hii inatengeneza vizazi vya waraibu wa dawa za kulevya hivyo wanawake walioathirika na dawa za kulevya kujitokeza ili wapatiwe matibabu katika vituo vilivyoanzishwa na Serikali.

Elimu juu ya dawa za kulevya inaendelea kutolewa kwa umma kupitia njia mbalimbali ikiwemo vyombo vya habari, matukio ya kitaifa, semina, makongamano na mitandao ya kijamii. Utoaji wa elimu ni mkakati muhimu wa kupunguza matumizi haramu ya dawa za kulevya kwa makundi tofauti ya rika.

Imetolewa na,

Florence Khambi

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali

**Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya.**